

## Nafasi ya Tafsiri katika Ufundishaji wa Kiswahili: Mfano wa Ufundishaji wa Kiswahili katika Shule za Upili nchini Uganda

Sarah Ndanu M. Ngesu  
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

### Ikisiri

Makala haya yanaangazia maoni ya walimu na wajifunzaji kuhusu matumizi ya tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda. Suala mojawapo linalozua mgogoro miongoni mwa wasomi, wataalamu, walimu na wajifunzaji wa lugha ni matumizi ya tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni na ya pili. Wanafunzi walioshiriki walikuwa wa kidato cha kwanza na cha pili. Data ilichanganuliwa kwa kutumia nadharia ya umotishaji wa lugha iliyoasisiwa na Gardner (1985) na kuendelezwa na Dörnyei (1994). Matokeo yanaonesha kwamba tafsiri ina nafasi kubwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda. Aidha, imebainika kwamba tafsiri haiwezi kuepukika katika mazingira ya ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda. Hata, hivyo mbinu hii inapaswa kutumika pamoja na mbinu nyinginezo na kwa njia inayofaa.

Dhana Muhimu: tafsiri, ufundishaji, ujifunzaji, Kiswahili, Uganda

### Utangulizi

Suala mojawapo linalozua mgogoro miongoni mwa wasomi, wataalamu, walimu na wajifunzaji wa lugha ni matumizi ya tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni na lugha ya pili. Kwa karne nyingi, tafsiri imepuuzwa kama mbinu muhimu ya ufundishaji wa lugha kutokana na kuhusishwa kwake na mbinu ya tafsiri-sarufi iliyotumika katika ufundishaji wa Kilatini na Kiyunani. Hata hivyo, matumizi ya tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha yanarejea kwa kasi katika karne hii ya 21. Watafiti na wataalamu (Duff, 1989; Cook, 2018) wanaoshadidia matumizi ya tafsiri kama njia muhimu ya ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni wanakubaliana kwamba ni zana inayowasaidia wajifunzaji kuelewa maneno na dhana za lugha lengwa. Wanaendelea kudai kwamba tafsiri ina nafasi kubwa katika elimu ya uwililugha na inajitegemea kama taaluma ya kiakademia. Makala haya yamejikita katika kuonesha mitazamo ya walimu na wajifunzaji kuhusu matumizi ya tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda.

### Historia Fupi ya Tafsiri kama Mbinu ya Ufundishaji wa Lugha

Tafsiri kama mbinu ya ufundishaji wa lugha ilitumika sana katika karne ya 18 wakati lugha. Mbinu ya tafsiri-sarufi ilikuwa maarufu na ilitambulika kuwa mbinu rasmi. Wataalamu wa ufundishaji wa Kiyunani na Kilatini katika shule za Ujerumani kama vile Ploetz, Seidenstucker, Meidinger na Ollendorf walitumia tafsiri-sarufi kufundishia Kiyunani na Kilatini kuanzia mwaka wa 1783 hadi 1849 (Marques na Solís-Becerra, 2013). Kulingana na Siefert (2013), mbinu ya tafsiri-sarufi iliasisiwa huko Prussia na Meidinger mwaka 1783 na kuendelezwa na wafuasi wake wanne Seidenstucker, Ahn, Ollendorf na Ploetz, ambao ni wataalamu wa taaluma ya pedagogia katika ufundishaji wa lugha. Mwanzoni mbinu hii haikujulikana kama tafsiri-sarufi, dhana ya tafsiri-sarufi iliundwa na wanamapinduzi walioipinga.

Marques na Solís-Becerra wanaeleza kwamba tafsiri-sarufi ni mbinu ya ufundishaji iliyoasisiwa na wataalamu wa Kijerumani na baadaye kuendelezwa na wanaisimu wa Marekani. Katika karne ya 19 walimu wa Kiingereza pia walitumia tafsiri-sarufi kufundisha Kiyunani na Kilatini. Lengo kuu la matumizi ya Sarufi-Tafsiri lilikuwa kufundisha lugha kwa kutafsiri kaida na msamiati wa lugha Lengwa, yaani lugha inayofundishwa (Hull, 2018). Wanafunzi walitakiwa kutumia mbinu ya tafsiri sisisi ili kuimarisha uwezo wao wa kusoma na kuandika pamoja na kutafsiri kazi za kifasihi. Halikadhalika, tafsiri imetumiwa nchini Hispania kama njia muhimu ya ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni kuanzia mwishoni mwa karne ya 19 hadi sasa (Marques na Solís-Becerra, 2013).

Kulingana na Ivanova (2016) na Hull (2018), tafsiri-sarufi ilikuwa na umaarufu ikilinganishwa na mbinu nyingine za ufundishaji na ujifunzaji wa LgK kuanzia miaka ya 1840 hadi 1940. Wakishadidia maoni haya, wanazuoni Kalantari na Karimnia (2012), wanaeleza kwamba tafsiri ilitumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha bora kama vile Kilatini na Kiyunani. Baadaye tafsiri ilitumiwa kufundishia lugha za kisasa na hata hii leo katika maeneo mengi duniani kama vile Uchina, India, Pakistani, Urusi na Hispania mbinu hii hutumika kwa upana katika ufundishaji na ujifunzaji wa LgK. Hata hivyo, mbinu ya tafsiri-sarufi iliyotumiwa katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ilizua mijadala mikali kutokana na wanazuoni kupinga matumizi yake.

Mwishoni mwa karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20, kundi la wanazuoni waliojitambulisha kama wanamageuzi lilipinga matumizi ya tafsiri-sarufi katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha. Wanamageuzi waliongozwa na Wilhelm kuanzia mwaka wa 1850 hadi 1918. Wilhelm alitilia mkazo lugha ya mazungumzo kuliko lugha ya maandishi. Hivyo, mbinu ya moja kwa moja ilianza kutumiwa badala ya tafsiri-sarufi katika miaka ya 1900 (Kelly na Bruen, 2015). Mbinu hii ilianza kuwa maarufu huko Ujerumani na Ufaransa. Mbinu nyinginezo zilianza kuibuka zilizohusiana na mbinu ya moja kwa moja. Kwa mfano, mbinu ya kimawasiliano ilichangia pakubwa kupuuzwa kwa tafsiri-sarufi katika ufundishaji

wa lugha. Miongoni mwa wanazuoni wanamageuzi waliopinga matumizi ya tafsiri-sarufi ni Passy (1899), Sweet (1900), Howatt (1984), Omaggio (2001), Brown (2007) na Doff (2008).

Wataalamu hawa wanadai kwamba mbinu ya tafsiri-sarufi haitilii maanani vipengele vitatu muhimu vya ufundishaji na ujifunzaji wa lugha: stadi ya kuzungumza, uzingativu wa muundo wa lugha na mbinu changamani za mawasiliano (Vermes, 2010). Hata hivyo, wanaopinga mbinu ya tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha wanaonekana kuegemea katika kuhusisha tafsiri na mbinu ya tafsiri-sarufi iliyokuwa ikitumika katika ufundishaji wa Kilatini na Kiyunani. Wataalamu hawa hawatofautishi baina ya tafsiri-sarufi na tafsiri kama zana ya ufundishaji wa lugha ya kigeni (tafsiri kimawasiliano). Dhana hizi hutofautiana kutegemea; uamilifu, walengwa, lengo na mwasilishaji wa ujumbe. Kwa mfano, tafsiri kama zana ya ufundishaji wa LgK hutumiwa kurahisisha mawasiliano, kukuza umilisi na kutathmini uelewa wa mjifunzaji. Tafsiri-sarufi iliyotumiwa katika ufundishaji wa Kiyunani na Kilatini ilijikita katika tafsiri za matini kwa kuzingatia kaida za lugha lengwa. Pia, wanaopinga wana maoni finyu kuhusu tafsiri yanayojikita kwenye tafsiri ya matini na kukosa kuitambua tafsiri kama mchakato wa mawasiliano darasani.

Lengo kuu la matumizi ya tafsiri-sarufi lilikuwa kuwasaidia wajifunzaji kuelewa muundo na sarufi ya lugha. Aidha, mbinu hii ilihusu uchanganuzi kileksika na kisarufi wa matini bora na ilionekana kama hatua ya kuboresha mbinu ya kimapokeo ya Kiskola iliyokuwepo awali. Pia, tafsiri-sarufi ilitumika mara nyingi katika uchanganuzi wa matini za kifasihi ili kuwatayarisha wajifunzaji kuwa wasemaji bora na kama kigezo cha kuwatenganisha wanafunzi mahiri na wasio mahiri. Ni muhimu kueleza kwamba kuna tofauti kati ya mbinu ya tafsiri-sarufi katika ufundishaji wa lugha yaliyotumika wakati huo na mbinu ya tafsiri kimawasiliano inayotumika katika ufundishaji wa lugha nyingi.

Kutokana na mageuzi yaliyofanywa na wataalamu kama vile Viëtor (1882), Passy (1899), Sweet (1900) na Bloomfield (1933) tafsiri-sarufi iliondolewa katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni na/au lugha ya pili. Mbinu ya moja kwa moja na mbinu ya kimawasiliano ilianza kutumiwa na kuendelea kwa miongo mingi iliyopita (Cook, 2010). Mbinu ya mawasiliano inasisitiza umuhimu wa wanafunzi kuwa na umilisi wa mawasiliano pamoja na uwezo wa kueleweka na wazawa wa lugha wanayojifunza.

### **Tafsiri katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Lugha katika Karne ya 21**

Kulingana na Cook (2010 & 2018), kuna mwamko mpya wa kutetea kurejeshwa kwa tafsiri katika ufundishaji wa LgK. Wataalamu kadhaa wamejitokeza kuitetea na kuonesha umuhimu wa tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa LgK hususani lugha za ulaya. Tafiti mbalimbali zinaonesha kwamba licha ya kupingwa kwa matumizi ya tafsiri-sarufi katika ufundishaji na ujifunzaji wa LgK, mbinu ya tafsiri imeendelea kutumiwa na walimu, wanafunzi na wachapishaji. Tafiti hizi pia

zinaonesha kuwa tafsiri ndiyo mbinu inayotumika zaidi katika ufundishaji na ujifunzaji wa LgK na au Lg2. Marinac na Baric (2018) wanaeleza kwamba katika nchi ambazo tafsiri hutumiwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha kama vile China, India na Urusi, wajifunzaji huwa na umilisi wa hali ya juu wa lugha wanayojifunza. Vilevile, imebainika kwamba katika baadhi ya nchi ambazo tafsiri haitumiwi kufundisha lugha ya kigeni umilisi wa wajifunzaji ni wa kiwango cha chini. Hivyo, wanadai kwamba tafsiri ni mbinu muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni ikitumiwa kama mbinu mojawapo badala ya kutumiwa kama mkabala wa pekee kama ilivyotumiwa mbinu ya tafsiri-sarufi.

Kumedhihirika kuongezeka kwa machapisho kuhusu kurejeshwa kwa tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa LgK. Tafsiri imeanza kujitokeza kama shughuli ya kimawasiliano tofauti na tafsiri-sarufi. Kwa mfano, tarehe 9/9/2019 kulikuwa na Kongamano la tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha Jijini Cambridge nchini Uingereza. Tangazo lilitolewa tarehe 25/6/2019 na lilikuwa hivi:

*Conference on translation in language teaching and learning. Title: The Translation Turn: Current Debates on the Role of Translation in Language Teaching and Learning. Venue: Runcie Room, Faculty of Divinity, Sidgwick Site, West Road, Cambridge CB3 9BS. Translation in language teaching is currently undergoing a process of reassessment and revival. The increasingly diverse linguistic background of today's populations has led to new needs and challenges in foreign language classroom. Thus, the strict monolingualism in the target language that became dogma in the latter part of the 20th century has been replaced today by bi-, mult- and plurilingual approaches.*

Kongamano kuhusu tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha. Mada: Mabadiliko katika Tafsiri: Mijadala kuhusu Nafasi ya Tafsiri katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Lugha. Mahali: Chumba cha Runcie, Shule ya Divinity, Sidgwick Site, West Road, Cambridge CB3 9BS. Kwa sasa tafsiri katika ufundishaji wa lugha iko katika mchakato wa kufanyiwa tathmini na kurejeshwa katika ufundishaji wa lugha. Hali ya wingilugha duniani imechangia mahitaji mapya na changamoto mpya katika darasa la lugha ya kigeni. Hivyo, mbinu ya lugha moja iliyotawala ufundishaji wa LgK mwishoni mwa karne ya 20, nafasi yake imechukuliwa na mikabala ya lugha mbili au lugha zaidi ya mbili ambapo tafsiri inapaswa kutumika katika muktadha huu (Tafsiri yangu).

Kwa kurejelea nukuu hili, inadhihirika kwamba tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa LgK kwa sasa haiwezi kuepukika na ni eneo jipya ambalo linahitaji kufanyiwa utafiti. Jambo hili linaungwa mkono na Ito (2017) na Karimah (2020) wanaoshadidia kwamba tafsiri haiwezi kuepukika katika ujifunzaji wa lugha ya kigeni. Hivyo, inadhihirika kwamba licha ya kupingwa kwa matumizi ya tafsiri katika ufundishaji wa lugha ya kigeni kutokana na uhusiano wake na tafsiri-sarufi,

tafsiri imeendelea kutumiwa katika maeneo mbalimbali duniani. Panda (2018) anaeleza kwamba tafsiri hutumiwa katika ufundishaji wa Kiingereza, Kihindi na Kisanskriti nchini India. Aidha, Liu (2019) anaeleza kwamba tafsiri hutumiwa katika shule, vyuo na vyuo vikuu vinavyofundisha Kiingereza kama lugha ya kigeni nchini China. Akishadidia hali hii, Pintado (2018) anaeleza kwamba tangu miaka ya 2000 kumedhihirika kushamiri kwa machapisho kuhusu kurejeshwa kwa tafsiri katika ufundishaji wa LgK. Tafsiri imeanza kujitokeza kama shughuli ya kimawasiliano tofauti na tafsiri-sarufi iliyopingwa na kuzua mjadala endelevu. Pintado anadai kwamba hata kama tafsiri imepuuzwa katika mitaala lakini inatumika katika shughuli halisi za ufundishaji wa LgK. Hali hii imedhihirika katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda ambapo tafsiri ya kimawasiliano hutumika kwa kiwango cha juu katika ufundishaji wa Kiswahili. Ingawa tafsiri haitambuliwi katika mtaala kama mbinu mojawapo ya ufundishaji wa Kiswahili, tafsiri hutumika zaidi kuliko mbinu nyinginezo. Mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili nchini Uganda ni tofauti na mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika nchi kama vile Kenya na Tanzania. Wajifunzaji hawapati ingizo kutoka kwa jamii kwa sababu Kiswahili hakizungumzwi na wanajamii wengi nchini Uganda tofauti na nchi zilizotajwa ambapo Kiswahili huzungumzwa na wanajamii wengi. Pia, katika nchi hizo Kiswahili ni lugha ya taifa na rasmi kiutendaji na wala si kinadharia.

### **Hali ya Ufundishaji wa Kiswahili Nchini Uganda iliyo Chachu ya Matumizi ya Tafsiri**

Kwa mujibu wa Jjingo na Vasser (2017) na Muhtasari wa Ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda (*Kiswahili Teaching Syllabus, 2008 na 2013*), Kiswahili kilianza kufundishwa na kutahiniwa nchini Uganda kabla ya uhuru bila muhtasari wa kuongoza ufundishaji na ujifunzaji huo. Chombo cha kutahini wakati huo kilikuwa *Cambridge Overseas Examination Council Syndicate*. Baadaye utahini ukawekwa chini ya *East Africa Examination Council*. Ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kabla ya uhuru haukuwa na umaarufu kwa wanafunzi kwa muda mrefu. Kwa mujibu wa Mukama (1989), hali hii ilibadilika kutokana na wanafunzi wengi kuvutiwa kusoma Kiswahili. Hali ya kuchangamkia ujifunzaji wa Kiswahili imetokana na umuhimu na dhima ya Kiswahili kikanda na kimataifa. Aidha, kufufuliwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na mtazamo chanya wa Serikali ya Uganda kwa sasa kuhusu Kiswahili umechangia kuwepo kwa mwamko mpya kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili nchini Uganda.

Kwa mujibu wa maelezo katika Muhtasari wa Ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda, lengo kuu la ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili nchini Uganda limechochewa na mambo manne. Kwanza, Kiswahili ni lugha ya mawasiliano mapana na mojawapo ya lugha chache za Afrika ambazo zinazungumzwa duniani. Pili, Kiswahili ni lugha mojawapo miongoni mwa lugha zinazoonesha maendeleo makubwa na ya kasi duniani. Tatu, Kiswahili ni lugha rasmi ya Jumuiya ya Afrika

Mashariki. Na mwisho, serikali ya Uganda inatambua umuhimu wa Kiswahili kama lugha ya kikanda na kimataifa inayoweza kuwaunganisha wananchi wa Uganda.

Ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili nchini Uganda umechochewa vilevile na hali ya kiisimu ya Uganda ya wingilugha na umoja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kuna lugha zaidi ya 43 za asili nchini Uganda na wanafunzi huzungumza lugha moja au mbili kati ya lugha hizi. Kiingereza hutumiwa kufundishia masomo yote kutoka darasa la nne (shule za msingi) hadi kidato cha sita na vilevile Chuo Kikuu. Kiingereza pia ni somo la lazima na kina hadhi ya lugha ya tabaka la juu pamoja na la wasomi (Masengo, 2018). Masengo anaeleza kwamba mwanzoni ni shule chache sana zilizokuwa zinafundisha somo la Kiswahili. Kufikia sasa, Kiswahili hufundishwa katika shule chache vijijini na mijini kutoka kidato cha kwanza hadi cha sita kama somo la hiari. Katika hali hii, wanafunzi wanaosoma Kiswahili huwa wana uwingilugha baina ya lugha zao za asili na Kiingereza. Pia, wanafunzi hujifunza Kiingereza kabla ya Kiswahili. Hali hii huchochea walimu kutumia tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza ili wajifunzaji waweze kuelewa dhana za Kiswahili. Kwa sababu hii, Kiswahili ni lugha ya kigeni nchini Uganda na hufundishwa katika kundi moja na wakati mmoja na lugha kama vile Kijerumani, Kifaransa na Kiarabu. Hivyo, wanafunzi huchagua kusoma lugha mojawapo.

Stern na wenzie (1983) na Philipo (2019) wanaeleza kwamba lugha ya kigeni ni lugha ambayo si lugha ya kwanza ya watu wengi katika nchi fulani. Wataalamu hawa wanaendelea kueleza kuwa lugha ya kigeni haitumiwi katika: kufundishia, mawasiliano ya kiserikali, vyombo vya habari, na katika mawasiliano ya wananchi ya kila siku. Katika makala haya, Kiswahili nchini Uganda hufundishwa kama LgK kwa sababu; mosi, Kiswahili si lugha ya asili kwa wakazi wa Uganda na haizungumzwi na wananchi wengi. Pili, Kiswahili hakitumiwi katika mawasiliano ya kila siku nchini Uganda. Tatu, wajifunzaji asilia (watu wa mwambao wa pwani ya Kenya na Tanzania na Visiwa vya Lamu, Pate, Pemba na Unguja) wa Kiswahili wako mbali na wajifunzaji wa Kiswahili nchini Uganda. Nne, Kiswahili ni lugha ya taifa kinadharia na wala si kiutendaji nchini Uganda. Tano, wajifunzaji wa Kiswahili nchini Uganda hujifunza katika muktadha rasmi wa darasani kwa sababu Kiswahili hakizungumzwi na watu wengi nje ya darasa. Hivyo, wajifunzaji wanakuwa na fursa kidogo au hukosa kabisa fursa ya kutumia lugha ya Kiswahili katika mazingira halisi ya mawasiliano asilia. Matumizi ya mbinu ya tafsiri huhusishwa na ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni.

### **Muktadha wa Kijamii na Mkabala wa Kinadharia**

Makala haya yamemutadhiswa nchini Uganda katika Jiji la Kampala ambalo ni mji mkuu wa Uganda. Kuna mambo kadhaa yaliyopelekea kuteuliwa kwa Jiji la Kampala. Mosi, eneo hili lina shule za sekondari zinazofundisha lugha ya Kiswahili. Pili, utafiti wa awali ulibainisha kwamba shule za sekondari Jijini Kampala hudahili wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali, ndani na nje ya Uganda.

Uchangamani huo wa wanafunzi huwalazimu walimu kutafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza na si lugha nyinginezo. Hali hii inashadidiwa na Masengo (2018) anayeeleza kwamba wajifunzaji wa Kiswahili nchini Uganda hutoka ndani na nje ya Afrika Mashariki. Jiji la Kampala imegawika katika tarafa tano: Kampala Kati, Makindye, Kawempe, Rubaga na Nakawa.

Shule za sekondari zilizochunguzwa katika utafiti huu ni za aina mbili, yaani shule za umma na shule za binafsi. Kwa ujumla, shule saba (7) ziliteuliwa katika jiji la Kampala. Shule hizo 7 ziliteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Hii ni kwa sababu ijapokuwa Kiswahili hufundishwa kama somo nchini Uganda, wakati wa utafiti huu, si shule zote zilizokuwa zikifundisha lugha hiyo. Kwa hivyo, shule hizi ziliteuliwa kwa msingi kwamba zinafundisha lugha ya Kiswahili. Miongoni mwa shule hizi saba (7), tuliteua shule moja moja kutoka tarafa tatu (Kampala Kati, Rubaga na Nakawa) na shule mbilimbili kutoka tarafa mbili ambazo ni Makindye na Kawempe. Uteuzi wa shule mbilimbili katika tarafa ya Makindye na Kawempe ulitokana na sababu kwamba zina shule nyingi zinazofundisha Kiswahili. Walimu na wanafunzi wa shule hizo saba walishirikishwa katika kujaza hojaji na pia walimu kutoka shule nyingine jijini humo. Hivyo, walengwa wa utafiti walikuwa walimu waliokuwa wakifundisha Kiswahili kidato cha kwanza na cha pili wakati wa utafiti na wanafunzi waliokuwa wakisoma Kiswahili kidato cha kwanza na cha pili wakati wa utafiti.

Wanafunzi wa kidato cha kwanza na cha pili waliteuliwa kwa kuwa wakati wa utafiti huu (2018 na 2019), Kiswahili kilikuwa kikifundishwa kama somo la lazima au la hitiari (hiari) katika ngazi hizo. Ilibainika kwamba katika shule chache Kiswahili ni somo la lazima kwa kidato cha kwanza (S1) na kidato cha pili (S2). Sampuli ya utafiti huu ilihusisha watoataarifa mia tatu thelathini na sita (336). Miongoni mwa hao ni walimu wanaofundisha Kiswahili arobaini na nane (48) na wanafunzi ni mia mbili na themanini na nane (288).

Data iliyotuiwa katika kuandaa makala haya ilikusanywa kupitia mbinu ya hojaji. Mwandishi wa makala haya aliandaa hojaji aina mbili zilizokuwa na maswali funge na maswali wazi. Mbinu hii ilichaguliwa kutokana na manufaa yake. Mosi, hojaji iliwezesha kukusanya data katika shule saba (7) katika tarafa tano (5) tofauti kwa haraka. Pili, ilisaidia kukusanya data kutoka katika sampuli kubwa. Tatu, iliwapu uwezo watoataarifa wa kujieleza kwa uwazi bila kuathiriwa na mtafiti. Kuhusu maswali-funge, watoataarifa walitakiwa kuchagua majibu yaliyokuwa yameorodheshwa. Maswali-wazi, yalilenga kuwapa watoataarifa nafasi ya kuelezea maoni yao wenyewe bila kudhibitiwa. Kulingana na Creswell (2018) maswali haya humwezesha mtafiti kuelewa na kutambua maoni ya watoataarifa vile yalivyo bila kuyaathiri kwa njia yoyote. Sehemu ya kwanza ilihusu taarifa binafsi za mtoa taarifa. Walimu walioshiriki katika kujaza hojaji walikuwa arobaini na nane (48) kutoka shule 38 za sekondari zinazofundisha Kiswahili Jijini Kampala.

Hojaji kwa wanafunzi ilitafsiriwa kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza baada ya watafiti kubaini kwamba wanafunzi hawakuweza kuelewa Kiswahili. Hojaji kwa

walimu iliandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Matokeo ya hojaji yalichambuliwa, kuchanganuliwa na kufasiriwa.

Makala haya yanaongozwa na Nadharia ya Umotishaji wa Lugha. Dhana ya motisha katika ujifunzaji wa lugha ya kigeni na lugha ya pili iliasisiwa katika miaka ya 1950 na wanasaikolojiajamii wawili yaani, Lambert na Gardner. Utafiti wao katika mwaka wa 1972 ulijenga msingi wa Nadharia ya Umotishaji katika Lugha. Mawazo ya Lambert na Gardner kuhusu nafasi ya motisha katika ufundishaji wa lugha yaliendelezwa na Gardner. Gardner aliunda Nadharia ya Umotishaji katika Lugha mwaka 1985. Utafiti huo uliwachochea wataalamu kufanya tafiti kuhusu motisha na ufundishaji wa LgK/Lg2. Baadhi ya wataalamu hao ni Zoltan Dörnyei ambaye aliasisi nadharia ya umotishaji mwaka 1994 kuhusu ufundishaji wa lugha ya pili. Hivyo, Nadharia ya Umotishaji iliyotumika kuchanganua data katika utafiti huu imezingatia maboresho yaliyofanywa na Dörnyei (1994). Kwa mujibu wa nadharia hii, kuna umotishaji unaotokana na somo au kozi. Umotishaji huu unahusu muhtasari wa somo/kozi unaotumiwa, vitendeakazi, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji na shughuli za darasani. Maoni haya yanaafikiana na maelezo ya wataalamuwa Lg2 na LgK (William, 1994; Chambers, 1999; Gardner na wenzie, 2004; Alshengeeti, 2018; Donyei & Muir, 2019) kwamba ufanisi katika ujifunzaji wa Lg2 na LgK hutegemea kinachofundishwa (maudhui) na mbinu za ufundishaji. Aidha kuna umotishaji unaotokana na mwalimu, yaani tabia yake, hulka yake, haiba yake, mtindo wake wa ufundishaji, uhusiano na wajifunzaji na mbinu anazotumia katika ufundishaji wa Lg2 au LgK. Pia kuna aina nyingine ya umotishaji inaohusiana na kundi zima, yaani malengo yao kama darasa kwa lugha wanayojifunza, ushirikiano wao na ushikamani wao.

Katika ufundishaji wa lugha ambayo wajifunzaji hawapati ingizo kutoka kwa jamii, walimu wanahitajika kuwapa motisha wanafunzi ili wafurahie kujifunza lugha hiyo. Kupitia data iliyojenga msingi wa makala haya, imebainika kwamba walimu wanaofundisha Kiswahili kidato cha 1 na kidato cha pili katika shule za sekondari nchini Uganda hutumia tafsiri kama njia ya kuwapa motisha wanafunzi ili waweze kufurahia kujifunza Kiswahili.

### **Matokeo na Mjadala**

Sehemu inayofuata inahusu matokeo ya utafiti na mjadala wa matokeo hayo. Kwa kuwa mbinu ya tafsiri hutumika katika mazingira ambayo wajifunzaji hawatumii lugha lengwa katika mawasiliano yao ya kila siku, ilionekana ni muhimu kubaini iwapo wajifunzaji waliweza kujifunza Kiswahili katika shule ya msingi. Taarifa hizi zilitarajiwa kusaidia katika kuibua masuala muhimu kuhusu umuhimu wa tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili nchini Uganda. Matokeo yanaonesha kwamba kati ya wanafunzi 288 walioshiriki, wanafunzi 252, sawa na 88% hawakusoma Kiswahili katika shule ya msingi. Ni wanafunzi 36 tu sawa na 12% waliosoma Kiswahili katika shule ya msingi. Hivyo, wanafunzi wengi huanza kujifunza Kiswahili katika shule ya sekondari.




Ili kupata maoni ya watoa taarifa (wajifunzaji na walimu) kuhusu matumizi ya tafsiri na kufaa kwake katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Madarasa yaliyolengwa yalikuwa ya kidato cha kwanza na cha pili ambayo wanafunzi huanza kusoma somo la Kiswahili. Jumla ya wanafunzi 288 na walimu 48 walishiriki kama watoataarifa katika utafiti huu. Watoataarifa walipewa hojaji iliyokuwa na maswali-funge ambayo yaliwahitaji kuchagua jibu moja miongoni mwa majibu waliyopewa. Hojaji pia ilikuwa na maswali-wazi ambayo yaliwataka watoataarifa kutoa maoni yao. Kuhusu maswali-funge katika hojaji kwa wanafunzi, swali la mojawapo liliwataka kuonesha kiasi ambacho mwalimu hutumia tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza katika ufundishaji wa Kiswahili. Swali jingine liliwataka kuonesha iwapo wao huelewa Kiswahili mwalimu akifundisha kwa kutumia Kiswahili pekee au akitumia tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Kuhusu maswali-wazi, swali mojawapo liliwataka kutoa sababu za kufurahia kusoma Kiswahili mwalimu akitumia mbinu waliyochagua.

Kuhusu hojaji kwa walimu, swali moja lililenga kubaini kiwango cha matumizi ya tafsiri katika ufundishaji wa Kiswahili nchini kwa mwalimu binafsi. Hivyo, swali hili liliuliza: *Kwa maoni yako, unadhani tafsiri hutumiwa na walimu nchini Uganda kama njia mojawapo ya kufundishia Kiswahili kwa kiwango gani?* Swali jingine liliuliza: *Mara nyingi unatumia mbinu gani kufundisha Kiswahili?* Maswali hayo yote mawili yalikuwa funge. Aidha, walimu walipewa maswali wazi mengine mawili ili kuwapa uhuru wa kujieleza. Swali moja liliuliza: *Ni sababu gani zinazochangia kutumia tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili?* Swali la pili liliuliza: *Je, ni mbinu gani unayofikiri ina manufaa zaidi katika ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda?*

Majibu ya watoataarifa yaliyojadiliwa ni yale tu yaliyoonekana kujibu maswali ya utafiti kwa kuafikiana na lengo la makala haya. Majibu yaliyoonekana kufanana au kukaribiana yaliwekwa pamoja na kuunda jumla ya maoni yaliyooneshwa. Matokeo ya maoni hayo yamewasilishwa katika majedwali na vielelezo.

### **Maoni ya Wanafunzi Kuhusu Kiwango cha Matumizi ya Tafsiri katika Ufundishaji wa Kiswahili**

Ili kupata maoni ya wanafunzi, walihitajika kujibu swali lifuatalo. *Onesha kwa alama ya kukubali kiasi anachotumia mwalimu tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza.* Walitakiwa kuchagua baina ya ‘mara nyingi’, ‘mara chache’ na ‘hatumii.’ Matokeo yanaonesha kwamba kati ya wanafunzi 288 walioshiriki, wanafunzi 195, sawa na 68%, walisema mwalimu hutumia tafsiri mara nyingi, wanafunzi 90, sawa na 31%, wakasema hutumia mara chache na ni wanafunzi 3 tu, sawa na 1%, waliosema mwalimu hatumii tafsiri katika ufundishaji wa Kiswahili. Kielelezo Na.1 kinaonesha ukokotoaji wa asilimia ili kutoa muhtasari na kumrahisishia msomaji kuelewa.




**Kielelezo Na. 1: Maoni ya Wanafunzi kuhusu Kiwango cha Matumizi ya Tafsiri katika Ufundishaji wa Kiswahili**

**Chanzo:** Data za Uwandani (2018/2019)

Matokeo haya yanaonesha kwamba tafsiri hutegemewa kama njia muhimu katika ufundishaji wa Kiswahili kwa kuwa wajifunzaji hawana nafasi ya kupata ingizo kutoka kwa wanajamii. Maoni ya wanafunzi yanalingana na maoni ya walimu kama inavyoonekana katika sehemu ifuatayo.

**Maoni ya Walimu Kuhusu Kiwango cha Matumizi ya Tafsiri katika Ufundishaji wa Kiswahili**

Ili kupata maoni ya walimu kuhusu kiwango cha matumizi ya tafsiri katika ufundishaji wa Kiswahili nchini kwa mwalimu binafsi, walipewa swali lifuatalo. *Kwa maoni yako, unadhani tafsiri hutumiwa na walimu nchini Uganda kama njia mojawapo ya kufundishia Kiswahili kwa kiwango gani?* Matokeo yalikuwa kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 2.



**Kielelezo Na. 2: Kiwango cha Matumizi ya Tafsiri katika Ufundishaji wa Kiswahili**

**Chanzo:** Data za Uwandani (2018/2019)

Kielelezo Na. 2 kinaonesha kwamba kati ya watoa taarifa (walimu) 48, watoataarifa 26, sawa na 54%, walisema tafsiri hutumiwa kwa kiwango cha juu sana. Vilevile, watoataarifa 8, sawa na 17%, walisema tafsiri hutumiwa sana, wengine 5, sawa na 10%, wakasema tafsiri hutumiwa kwa wastani, watoataarifa 4, sawa 8%, wakasema kwamba tafsiri hutumiwa kwa kiwango kidogo na 5, sawa 10%, wakasema hutumiwa kwa kiwango kidogo sana. Swali hili liliniwa kutoa taswira ya jumla ya matumizi ya tafsiri katika ufundishaji wa Kiswahili na yalioana na maoni ya swali lililolenga mwalimu binafsi kama inavyodhihirika katika matokeo yafuatayo.

Swali jingine katika hojaji liliuliza: *Mara nyingi unatumia mbinu gani kufundisha Kiswahili?* Hili lilikuwa swali funge na watoataarifa walitakiwa kuchagua jibu mojawapo. Matokeo yanaoneshwa katika Jedwali Na. 1.

**Jedwali Na. 1: Njia Watumiayo Walimu Mara Nyingi katika Ufundishaji wa Kiswahili**

Jumla ya Walimu watoataarifa	Tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza	Kiswahili Pekee	Mbinu Nyingine	Tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza pamoja na mbinu nyingine	Tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza pamoja na matumizi ya Kiswahili pekee
48	34	4	0	6	4

**Chanzo:** Data za Uwandani (2018/2019)

Jedwali Na. 1 linaonesha kwamba kati ya watoa taarifa 48 walioshiriki, 34 walisema mara nyingi hutumia tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza, watoataarifa 4, wakasema mara nyingi hutumia Kiswahili pekee, watoataarifa 6, wakasema hutumia tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza pamoja na mbinu nyingine, 4 wakasema hutumia tafsiri pamoja na Kiswahili pekee; hakuna aliyesema hutumia mbinu nyingine. Hali hii inadhihirisha utegemezi wa tafsiri wa kiwango cha juu katika ufundishaji wa Kiswahili.

Maoni ya wanafunzi na walimu kuhusu kiwango cha matumizi ya tafsiri kwa ujumla katika ufundishaji na ujifunzaji yanaonesha kwamba mbinu ya tafsiri hutumiwa kwa kiwango cha juu katika ufundishaji wa Kiswahili. Mtokeo haya yana maana kwamba kuna haja ya kutathmini mtaala kuhusu mbinu za ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda. Kama ilivyoenezwa awali, tafsiri haitambuliwi kama mbinu ya ufundishaji wa Kiswahili ingawa ndio njia inayotumika kwa kiwango cha juu. Pia, matokeo haya yana maana kwamba kuna umuhimu wa kutathmini tafsiri zinazofanywa ili kuepuka athari hasi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili.

Ilionekana muhimu kupata maoni ya watoataarifa (walimu) kuhusu mbinu wanayofikiria inafaa katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Swali mojawapo katika hojaji liliuliza, *Je, ni mbinu gani unayofikiria ina manufaa zaidi katika ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda?* Swali hili lilikuwa wazi. Hivyo, walimu

walikuwa huru kuonesha mbinu waliyofikiria inafaa katika kufanikisha ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda. Matokeo yanaoneshwa katika Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2: Maoni ya Walimu kuhusu Njia iliyo na Manufaa zaidi katika Ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda**

Jumla ya Watoaarifa 48	Tafsiri Kutika Kiswahili kwenda Kiswahili Pekee	Maonyesho	Utendaji	Majadiliano	Mbinu ya Kimawasiliano	Ugizaji	
	34	5	2	1	3	2	1
<b>Asilimia (%)</b>	71%	10%	4%	2%	6%	4%	2%

**Chanzo:** Data za Uwandani, 2018/2019

Data katika Jedwali Na. 2 inaonesha kwamba kati ya walimu 48 walioshiriki, 34 sawa na 71 % walisema tafsiri inafaa katika ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda, 5 sawa na 10% wakasema mbinu inayofaa ni Kiswahili pekee, watoaarifa 3 sawa na 6 % wakasema majadiliano, watoaarifa 2 sawa na 4% wakasema ni maonyesho, watoaarifa 2 sawa na 4% wakasema mbinu ya kimawasiliano, mtoaarifa 1 sawa na 2% akasema utndaji na mtoaarifa 1 sawa na 2% akasema ugizaji. Hivyo, mbinu ya tafsiri ilionekana kutajwa na watoaarifa wengi (71%) kuwa inafaa katika ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda.

Ili kupata maoni zaidi kuhusu matumizi ya tafsiri katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda, mtafiti alitunga swali wazi ambalo walimu waliweza kutoa maoni yao kuonesha kufaa kwa tafsiri. Swali hili liliuliza: *Kwa maoni yako eleza kwa nini mninu uliyochagua unadhani inafaa katika ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda. Kama ilivyooneshwa awali, walimu wengi walichagua mbinu ya tafsiri na kutoa sababu zifuatazo kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 3. Jedwali Na. 3 linaonesha hoja zilizotolewa na walimu kuhusu sababu zao za kufikiria matumizi ya tafsiri inafaa katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili nchini Uganda. Watoaarifa wote 48 walisema kuwa wanafunzi hawaelewi wanapofundishwa kwa Kiswahili pekee bila kutafsiri. Watoaarifa 44 sawa na 92% wakasema tafsiri ni mojawapo wa mada zinazofundishwa na kutahiniwa. Hivyo, wanapotafsiri darasani huwaandaa wanafunzi kukabiliana na sehemu ya tafsiri katika mtihani. Pia, watoaarifa 44 sawa na 88% wakasema hutumia tafsiri ili kuwapa wanafunzi msukumo kwa kuwa wengi wao wana mtazamo hasi kuhusu Kiswahili. Matokeo haya yanaonesha kwamba walimu 40 sawa na 83% walisema kwamba wanafunzi wengi wanasoma Kiswahili kwa mara ya kwanza wakiwa kidato cha kwanza. Halikadhalika, watoaarifa 31 ambao ni 65 % wakasema kuwa wanafunzi huelewa lugha ya Kiingereza kwa kuwa*


wanajifundisha kutoka utotoni. Hivyo, walimu hutafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza ili kurahisisha mawasiliano. Pia, watoataarifa 30 ambao ni 63 % wakasema Kiswahili ni lugha ya kigeni kwa wanafunzi wengi.

**Jedwali Na. 3: Maoni ya Walimu Kuhusu Tafsiri katika Ufundishaji Kiswahili**

<b>Jumla ya Watoataarifa 48</b>	<b>Sababu</b>	<b>Idadi ya Watoataarifa</b>	<b>Asilimia (%)</b>
	Wanafunzi hawaelewi wanapofundishwa kwa Kiswahili pekee bila kutafsiri.	<b>48</b>	100%
	Tafsiri ni mojawapo wa mada zinazofundishwa na kutahiniwa.	<b>44</b>	92%
	Ili kuwapa wanafunzi msukumo wengi wao wana mtazamo hasi kuhusu Kiswahili.	<b>42</b>	88%
	Wanafunzi wengi wanasoma Kiswahili kwa mara ya kwanza wakiwa kidato cha kwanza.	<b>40</b>	83%
	Wanafunzi huelewa lugha ya Kiingereza kwa kuwa wanajifundisha kutoka utotoni.	<b>31</b>	65%
	Kiswahili ni lugha ya kigeni kwa wanafunzi wengi.	<b>30</b>	63%
	Baadhi ya walimu hawana umahiri wa kutosha wa kuongea Kiswahili kwa muda mrefu.	<b>19</b>	40%
	Mtalaal kutokana na muundo wa karatasi za mitihani.	<b>8</b>	17%
	Ukosefu wa vitendea kazi/vitabu vilivyotafsiriwa au kuandikwa kwa Kiswahili pekee.	<b>6</b>	13%

**Chanzo:** Data za Uwandani, 2018/2019

Ili kupata maoni ya wanafunzi kuhusu njia wanayofurahia na ambayo huwasaidia kuelewa kwa urahisi mwalimu anapoitumia kufundisha Kiswahili, swali mojawapo liliuliza: *Unafurahia kusoma Kiswahili mwalimu akitumia njia gani anapofundisha?* Wajifunzaji walitakiwa kuchagua jibu moja kati ya; *kutumia Kiswahili pekee na kutumia tafsiri ya Kiswahili kwenda Kiingereza.* Matokeo yalikuwa kama yanavyooneshwa katika Kielelezo Na.3.



**Kielelezo Na. 3: Maoni ya Wanafunzi kuhusu Njia Wanayofurahia na Ambayo Huwasaidia Kuelewa kwa Urahisi**

**Chanzo:** Data za Uwandani, 2018/2019

Kwa kurejelea Kielelezo Na. 3, inadhihirika kwamba kati ya wanafunzi 288 walioshiriki kujaza hojaji, wanafunzi 279 sawa na 97% walisema huelewa kujifunza Kiswahili mwalimu akitumia tafsiri na ni wanafunzi 9 tu sawa na 3% waliosema hufurahia mwalimu akitumia Kiswahili pekee. Hivyo, matumizi ya tafsiri huwasaidia kujifunza Kiswahili. Aidha, tulitaka kubaini sababu za wanafunzi wengi kufurahia kujifunza Kiswahili kupitia mchakato wa tafsiri. Ili kufikia utambuzi huu, swali jingine katika hojaji liliuliza; *'Toa sababu za jibu lako hapo juu.'* Wajifunzaji 97% waliosema hufurahia mwalimu akitumia tafsiri walitoa sababu zao kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 4. Jedwali Na. 4 linaonesha kwamba wanafunzi wote (288) walisema huelewa kusoma Kiswahili mwalimu akitafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza kwa sababu tafsiri hurahisisha mawasiliano na kuwafanya kuelewa dhana za Kiswahili. Wanafunzi 266 sawa na 92% walisema hufurahia tafsiri kwa sababu walianza kujifunza Kiingereza wakiwa wadogo hivyo wanakielewa Kiingereza vizuri. Hivyo, tafsiri kwenda Kiingereza huwafaa katika kurahisisha mawasiliano. Pia, wanafunzi 256 ambao ni 89% walisema wanafunzi wengi hawaelewi Kiswahili kwa kuwa hawakusoma shule ya msingi. Wanafunzi wengine 220 sawa na 76% walisema walianza kujifunza Kiswahili shule ya sekondari. Kwa hivyo, lugha ya Kiswahili ni lugha ya kigeni.

**Jedwali Na. 4: Maoni ya Wanafunzi kuhusu Sababu za kufurahia Mwalimu Akitumia Tafsiri katika Ufundishaji Kiswahili**

Na.	Sababu	Idadi ya wanafunzi	Asilimia
1	Wanafunzi wengi hawaelewi Kiswahili kwa kuwa hawakusoma shule ya msingi.	256	89%
2	Wanakutana na Kiswahili shule ya sekondari.	220	76%
3	Maneno mengine ya Kiswahili ni magumu.	100	35%
4	Walianza kujifunza Kiingereza wakiwa wachanga hivyo wanakielewa.	266	92%
5	Tafsiri hurahisisha mawasiliano na kuwafanya waelewe dhana za Kiswahili.	288	100%
6	Hufurahia kusoma Kiswahili mwalimu anapotumia tafsiri.	151	52%
7	Hurahisisha ujifunzaji wa msamiati wa Kiswahili.	187	65%
8	Husaidia katika ulinganishaji wa Kiswahili na Kiingereza ili kuepuka kufanya makosa.	147	51%
9	Huwapa msukumo wa kusoma Kiswahili.	77	27%
10	Huwawezesha kukabiliana na maswali ya tafsiri katika mtihani.	85	30%
11	Husaidia kukuza stadi za lugha.	92	32%
12	Huwezesha kujifunza lugha mbili kwa wakati mmoja.	44	15%

**Chanzo:** Data za Uwandani, 2018/2019

Kwa hivyo, ni wazi kuwa tafsiri kwa jumla hutumika kwa kiwango cha juu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili nchini Uganda. Aidha, matokeo yanaonesha kwamba mbinu ya tafsiri ina nafasi muhimu katika ufundishaji wa lugha kutegemea miktadha mahususi kama ilivvyo nchini Uganda. Mosi, tafsiri ni nyenzo ya kurahisisha mawasiliano baina ya mwalimu na mwanafunzi. Pili, tafsiri ilionekana kuwapa motisha wajifunzaji na kuwasaidia kukabiliana na mihemko ambayo inaweza kuwa na athari hasi katika ujifunzaji wa Kiswahili kama LgK. Tatu, tafsiri iliwasaidia walimu kutathmini uelewa wa wanafunzi. Ni muhimu kueleza kwamba tafsiri hutahiniwa kama sehemu mojawapo ya lugha ya Kiswahili katika mtihani wa kidato cha nne na cha sita nchini Uganda. Nne, walimu walitumia tafsiri ili kuwasaidia wanafunzi kukabiliana na mihemko. Hali hii imetokana na sababu kwamba wanafunzi hawaelewi wakifundishwa kwa Kiswahili pekee kwa kuwa baadhi yao hawakusoma Kiswahili katika shule ya msingi, wanafunzi hawapati ingizo kutoka nyumbani na katika mazingira ya nje ya darasa na Kiswahili ni kama lugha ya kigeni nchini Uganda.

Tano, matumizi ya tafsiri yaliwatayarisha wanafunzi kufanya mtihani wa tafsiri kama sehemu mojawapo ya lugha ya Kiswahili inayotahiniwa kulingana na mtaala nchini Uganda. Sita, matumizi ya tafsiri yalifaa kwa kuwapa motisha wajifunzaji kwa kuwa baadhi yao wanakutana na Kiswahili kwa mara ya kwanza. Hivyo,

imebainika kwamba katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni nchini Uganda, matumizi ya tafsiri hayawezi kuepukika katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili, kidato cha kwanza na cha pili.

### Hitimisho

Makala haya yanapalilia kauli isemayo kwamba tafsiri haiwezi kuepukika katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili hususan kidato cha kwanza na cha pili kwenye shule zilizo jijini Kampala. Pia, imebainika kwamba matumizi ya mbinu ya kimawasiliano inayopendekezwa na wataalamu haiwezi kufaa pekee yake katika muktadha wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili nchini Uganda. Hali na mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili nchini Uganda una sifa bainifu zinazolingana na ufundishaji wa Kifaransa na Kijerumani nchini Kenya na Tanzania. Aidha, imebainika kuwa matumizi ya tafsiri kama yanavyotumika nchini Uganda ni tofauti na mbinu ya tafsiri-sarufi iliyotumika hapo awali na ambayo inapingwa na baadhi ya wataalamu. Hata hivyo, kuna changamoto za tafsiri tenge zinazotokana na ujuzi wa walimu ambazo hazikujadiliwa kwa kuwa halikuwa lengo la makala haya. Inapendekezwa kuwa walimu waweze kuandaliwa vyema kwa kufundishwa kozi kadha za tafsiri na pia kuhusu mbinu za ufundishaji wa lugha ya kigeni na ya pili. Kila mbinu ya ufundishaji huwa na manufaa na udhaifu. Hivyo, inapendekezwa matumizi ya mbinu changamano ambazo zitaweza kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili.

### Marejeleo

- Abdul-Azim, H. O. M. (2017). "Use of Translation for Enhancing Learning Performance of Students at the University Level." Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Sudan cha Sayansi na Teknolojia (Haijchapishwa).
- Alshenqeeti, H. (2018). Motivation and Foreign Language Learning: Exploring the Rise of Motivation Strategies in the EFL Classroom. *International Journal of Applied Linguistics and English Literature*, 7(7), 1-8.
- Benzigar, M. (2019). Language Teaching Through Translation. *Language in India*. Chuo Kikuu cha Christ, Bangalore.
- Brown, H. D. (2007). *Principles of Language Learning and Teaching, 5<sup>th</sup> Edition*. White Plains, N.Y. Pearson Education.
- Chambers, G. N. (1999). *Motivating Language Learners* (Juz. 12). Clevedon: Multilingual Matters.
- Cook, G. (2010). *Translation in Language Teaching: An Argument for Reassessment*. Oxford: Oxford University Press.
- Cook, G. (2018). Learning Through Translation. Katika Burns, A. & Richards, J.C. (Wah.), *The Cambridge Guide to Learning English as a Second Language* (289-306). London: Cambridge University Press.



- Creswell, J. W. (2018). *Qualitative Inquiry & Research Design: Choosing among Five Approaches* (4th ed.). Thousand Oaks, CA: SAGE Publications.
- Doff, S. (2008). How Language Teaching Started Afresh: Origins and Repercussions in the Reform Movement in German Foreign Language Teaching Curricula. *Journal of the American Association for the Advancement of Curriculum Studies*, Vol. 4. Iliyosomwa tarehe 17/1/2020 katika <https://ojs.library.ubc.ca/index.php/jaaacs/article/view/187672/185771>
- Dörnyei, Z. (1994). Motivation and Motivating in the Foreign Language Classroom. *The Modern Language Journal*, 78(3), 273-284.
- Dörnyei, Z. (2019). From Integrative Motivation to Directed Motivational Currents: The Evolution of the Understanding of L2 Motivation over Three Decades. Katika Martin, I.; Kata, C.; Alastair, H.; & Stephen, R. *The Palgrave Handbook of Motivation for Language Learning* (39-69). Switzerland: Palgrave Macmillan, Cham.
- Dörnyei, Z., & Muir, C. (2019). Creating a Motivating Classroom Environment. *Second Handbook of English Language Teaching*, 719-736.
- Duff, A. (1989). *The translator's Handbook*. Oxford: Oxford University Press.
- Gardner, R. C (1985). *Social Psychology and Second Language Learning: The Role of Attitudes and Motivation*. London: Edward Arnold.
- Hull, T. (2018). Content Based Instruction: A communicative Approach for the EFL Classroom. *PUPIL. International Journal of Teaching, Education and Learning*, 2(3), 63-77.
- Hull, T. (2018). Content Based Instruction: A communicative Approach for the EFL Classroom. *PUPIL. International Journal of Teaching, Education and Learning*, 2(3), 63-77.
- Ito, K. (2017). *The Efficacy of Translation and Oral Corrective Feedback in Promoting Language Proficiency Development (Tasnifu ya Uzamivu)*. State University of New York at Binghamton.
- Ivanova, I. (2016). "Re-introducing Own-language Use, Code-switching and Translation in FL Classrooms through Intralingual Strategies and Approaches." *Eltam Journal*, 5-16.
- Jjingo, C., & Visser, M. (2017). The Ssenteza Kajubi Legacy: The Promotion of Teaching Kiswahili in Uganda. *Journal of Pan African Studies*, 10(9), 1-14.
- Kalantari, E., & Karimnia, A. (2012). The Application of a Translation Model to Foreign Language Teaching Methodology. *World Applied Sciences Journal*, 16(10), 1416-1426.
- Karimah, A. (2020). Revisiting Translation as a Foreign Language Learning Tool: Contrasting Beliefs of Diversely Proficient Students. *Saga: Journal of English Language Teaching and Applied Linguistics*, 1(1), 9-16.
- Liu, G. (2019). Language Sociality and Its Enlightenment on Foreign Language Teaching. *Theory and Practice in Language Studies*, 9(8), 978-983.

- Marinac, M., & Barić, I. (2018). Teachers' Attitudes toward and Use of Translation in the Foreign Language Classroom at Institutions of Higher Education in Croatia. *Theory and Practice in Language Studies*, 8(8), 906-915.
- Marqués A.T. & Solís-Becerra, J. A. (2013). An Overview of Translation in Language Teaching Methods: Implications for EFL in Secondary Education in the Region of Murcia. *Revista de Lingüística y Lenguas Aplicadas*, 8(1), 38-48.
- Masengo, I. J. (2018). *Cross-linguistic Influence in Third Language Production among Kiswahili Learners* (Tasnifu ya Uzamivu). Chuo Kikuu cha Makerere.
- Mtesigwa, P. (2009). Utayarishaji wa Vitabu vya Kufundishia Kiswahili kama Lugha ya Kigeni: Haja ya Kuzingatia Mkabala wa Mawasiliano. *Kiswahili*, 72(1):52-67.
- Mukama, R. (1989). Hali na Hadhi ya Kiswahili Nchini Uganda. Katika *Makala za Mkutano wa Kimataifa wa Usanifishaji wa Istilahi za Kiswahili*. University of Dar es Salaam: Taasisi ya Utafiti wa Kiswahili.
- Mwansoko, H.J. M., Mekacha, R. D. K., Masoko, D.L.W., & Mtesigwa, P.C.K. (2015). *Kitangulizi cha Tafiri: Nadharia na Mbinu*. Dar-es Salaam:TUKI.
- Omaggio, H. A. (2001). *Language Teaching in Context*. Boston: Heinle.
- Omar, Y. Z. (2019). Influence of Grammar Translation Method (GTM) on Libyan Students English Performance in Communicative Situations. *People: International Journal of Social Sciences*, 5(2). 511-530.
- Panda, A. K. (2018). Translation as a Part of School Curriculum in Learning English Language. *Language Circle: Journal of Language and Literature*, 12(2), 137-142.
- Pintado G. L. (2018). Translation in Language Teaching, Pedagogical Translation, and Code-Switching: Restructuring the Toundaries. *The Language Learning Journal*, 1-21.
- Philipo, Z.T. (2019). Tofauti za Ujifunzaji wa Lugha ya Pili na Lugha ya Kigeni: Mifano ya Lugha ya Kiswahili Nchini Tanzania na Ughaibuni. *Jarida la Kimataifa la Isimu ya Kibantu*, 224-241.
- Pym, A., & Ayvazyan, N. (2016). Linguistics, Translation and Interpreting in Foreign-Language Teaching Contexts.
- Siefert, T. R. (2013). Translation in Foreign Language Pedagogy: The Rise and Fall of the Grammar Translation Method (Tasnifu ya Uzamivu). Chuo Kikuu cha Harvard.
- Stern, H. H., Tarone, E. E., Stern, H. H., Yule, G., & Stern, H. (1983). *Fundamental Concepts of Language Teaching: Historical and Interdisciplinary Perspectives on Applied Linguistic Research*. London: Oxford University Press.
- Sweet, H. (1900). *The Practical Study of Languages: A Guide for Teachers and Learners*. New York: Henry Holt and Company.
- Vermes, A. (2010). Translation in Foreign Language Teaching: A Brief Overview of Pros and Cons. *Eger Journal of English Studies*, 10, 83-93.
- Viëtor, W. (1882/1902). *Die Methodik des neusprachlichen Unterrichts: Ein geschichtlicher Überblick in vier Vorträgen*. Leipzig: B.G. Teubner.